

KUMB: PPR/16 - 12/1

**TAARIFA KWA UMMA KUHUSU BEI KIKOMO ZA MAFUTA AINA YA PETROLI KUANZIA
JUMATANO, TAREHE 7 DESEMBA, 2016**

Mamlaka ya Udhibiti wa Huduma za Nishati na Maji (EWURA), inatangaza bei kikomo za bidhaa za mafuta ya petroli hapa nchini. Bei hizi zitaanza kutumika kuanzia **Jumatano, Tarehe 7 Desemba, 2016**. Pamoja na kutambua bei kikomo za bidhaa mbalimbali za petroli nchi nzima, ni muhimu kuzingatia yafuatayo:-

- (a) Bei za jumla na rejareja kwa mafuta ya aina zote yaani Petroli, Dizeli na Mafuta ya Taa zimebadilika ikilinganishwa na toleo lililopita la tarehe 2 Novemba 2016. Kwa Mwezi Desemba 2016, bei za rejareja kwa Petroli, Dizeli na Mafuta ya Taa zimeongezeka kama ifuatavyo: TZS 29/lita sawa na asilimia 1.59, TZS 78/lita sawa na asilimia 4.53 na TZS 68/lita sawa na asilimia 4.08 sawia. Vilevile, kwa kulinganisha na toleo la mwezi uliopita, bei za jumla kwa mafuta ya Petroli, Dizeli na Mafuta ya Taa nazo zimeongezeka kama ifuatavyo: TZS 29/lita sawa na asilimia 1.68, TZS 78/lita sawa na asilimia 4.84 na TZS 68/lita sawa na asilimia 4.36. Kuendelea kupanda kwa bei za mafuta kwenye soko la ndani, kwa kiasi kikubwa kumetokana na kupanda kwa bei za mafuta katika soko la dunia
- (b) Bei za jumla na za rejareja kwa mafuta ya Petroli na Dizeli kwa mkoa wa Tanga, nazo zimepanda isipokuwa Mafuta ya Taa ambapo bei imeshuka ikilinganishwa na toleo la bei za mafuta hayo lililopita la tarehe 02 Novemba 2016. Katika toleo hili, bei ya rejareja kwa Petroli na Dizeli zimepanda kama ifuatavyo: TZS 8/lita sawa na asilimia 0.43 na Dizeli kwa TZS 14/lita sawa na asilimia 0.80, kwa Mafuta ya Taa bei imepungua kwa TZS 3/lita sawa na asilimia 0.16. Aidha, kwa kulinganisha matoleo haya mawili, bei za jumla kwa mafuta ya Petroli na Dizeli mkoa wa Tanga zimepanda kwa TZS 8/lita sawa na asilimia 0.45 na Dizeli TZS 14/lita sawa na asilimia 0.86, na kwa Mafuta ya Taa bei imepungua kwa TZS 3/lita sawa na asilimia 0.17. Kupungua kwa bei ya Mafuta ya Taa kumesababishwa na kupungua zaidi kwa gharama ya usafirishaji (*premium*) na kuongezeka kidogo kwa bei ya mafuta haya katika soko la dunia ukilinganisha na mafuta ya Dizeli na Petroli.
- (c) Mamlaka inapenda kuukumbusha umma kwamba bei kikomo za mafuta kwa eneo husika, zinapatikana vile vile kupitia simu za mkononi kwa kupiga namba ***152*00#** na kisha kufuata maelekezo. Huduma hii ni bure na inapatikana kupitia mitandao yote ya simu za mkononi hapa nchini.
- (d) Kwa mujibu wa Sheria ya Mafuta ya mwaka 2015, bei za bidhaa za mafuta ya petroli zitaendelea kupangwa na soko. EWURA itaendelea kuhamasisha ushindani kwa kutoa taarifa za bei kikomo za bidhaa za mafuta. Taarifa hizi zina lengo la kuwasaidia wadau kufanya maamuzi stahiki kuhusu manunuzi ya bidhaa za mafuta.
- (e) **Kampuni za mafuta zipo huru kuuza bidhaa za mafuta ya petroli kwa bei ya ushindani mradi tu bei hizo ziwe chini ya bei kikomo (price cap)** kama ilivyokokotolewa na fomula iliyopitishwa na EWURA na ambayo ilichapishwa katika **Gazeti la Serikali Na. 70/2016 la Mwezi Februari 2016**.

- (f) Vituo vyote vya mafuta vinatakiwa kuchapisha bei za bidhaa za mafuta katika mabango yanayoonekana bayana na yakionesha bei ya mafuta, punguzo, vivutio vya biashara au promosheni zinazotolewa na kituo husika. Pale ambapo inawezekana kuchagua, wateja wanashauriwa kununua bidhaa za mafuta katika vituo vinavyouza mafuta kwa bei ndogo zaidi ili kushamirisha ushindani. **Ni kosa kuuza mafuta bila kuweka mabango ya bei inayoonekana vizuri kwa wateja. Adhabu kali itatolewa kwa kituo husika kwa kutotekeleza matakwa ya kisheria kwa mujibu wa kanuni husika.**
- (g) Wanunuzi wahakikishe wanapata stakabadhi ya malipo inayoonesha jina la kituo, tarehe, aina ya mafuta yaliyonunuliwa na bei kwa lita. Stakabadhi hiyo ya malipo itatumika kama kidhibiti cha mnunuzi wa mafuta endapo kutajitokeza malalamiko ya ama kuuziwa mafuta kwa bei ya juu kuliko bei kikomo au kuuziwa mafuta yenye kiwango cha ubora kisichofaa

A: BEI ZA REJAREJA

Mji	Bei Kikomo		
	Petroli (Sh/Lita)	Dizeli (Sh/lita)	Mafuta Ya Taa (Sh/Lita)
Dar es Salaam	1,890	1,798	1,737
Arusha	1,974	1,882	1,821
Arumeru (Usa West)	1,974	1,882	1,821
Karatu	1,992	1,900	1,839
Monduli	1,979	1,887	1,826
Monduli-Makuyuni	1,984	1,892	1,831
Ngorongoro (Loliondo)	2,065	1,973	1,912
Kibaha	1,894	1,803	1,741
Bagamoyo	1,901	1,809	1,748
Kisarawe	1,897	1,805	1,744
Mkuranga	1,900	1,808	1,747
Rufiji	1,917	1,826	1,764
Dodoma	1,948	1,857	1,796
Bahi	1,956	1,864	1,803
Chemba	1,975	1,883	1,822
Konooa	1,981	1,890	1,828
Kongwa	1,946	1,854	1,793
Mpwapwa	1,950	1,858	1,797
Iringa	1,954	1,862	1,801
Kilolo	1,958	1,867	1,805
Mufindi (Mafinga)	1,964	1,872	1,811
Njombe	1,982	1,890	1,829
Ludewa	2,020	1,928	1,867
Makete	2,013	1,921	1,860
Wanging'ombe (Igwachanya)	1,980	1,888	1,827
Bukoba	2,105	2,013	1,952

Biharamulo	2,079	1,987	1,926
Karagwe (Kayanga)	2,121	2,029	1,968
Kyerwa (Ruberwa)	2,127	2,035	1,974
Muleba	2,105	2,013	1,952
Ngara	2,070	1,979	1,917
Misenyi	2,113	2,022	1,960
Geita	2,055	1,963	1,902
Bukombe	2,044	1,952	1,891
Chato	2,076	1,984	1,923
Mbogwe	2,093	2,001	1,940
Nyang'hwale	2,070	1,978	1,917
Kigoma	2,121	2,029	1,968
Uvinza (Lugufu)	2,133	2,041	1,980
Buhigwe	2,110	2,018	1,957
Kakonko	2,078	1,986	1,925
Kasulu	2,107	2,015	1,954
Kibondo	2,085	1,993	1,932
Moshi	1,963	1,872	1,811
Hai (Bomang'ombe)	1,967	1,875	1,814
Mwanga	1,956	1,865	1,804
Rombo (Mkuu)	1,984	1,893	1,831
Same	1,950	1,858	1,797
Siha (Sanya Juu)	1,970	1,878	1,817
Lindi	1,949	1,857	1,796
Lindi-Mtama	1,967	1,875	1,814
Kilwa Masoko	1,924	1,832	1,771
Liwale	1,969	1,878	1,817
Nachingwea	1,978	1,886	1,825
Ruangwa	1,979	1,888	1,826
Babati	2,012	1,920	1,859
Hanang (Katesh)	2,022	1,931	1,870
Kiteto (Kibaya)	2,023	1,931	1,870
Mbulu	2,025	1,933	1,872
Simanjiro (Orkasumet)	2,044	1,952	1,891
Musoma	2,068	1,976	1,915
Musoma Vijijini (Busekela)	2,109	2,017	1,956
Rorya (Ingirijuu)	2,077	1,985	1,924
Rorya (Shirati)	2,111	2,020	1,959
Bunda	2,059	1,967	1,906
Butiama	2,065	1,973	1,912
Serengeti (Mugumu)	2,113	2,022	1,961
Tarime	2,079	1,987	1,926
Mbeya	1,997	1,905	1,844
Chunya	2,006	1,915	1,853
Chunya (Makongolosi)	2,020	1,929	1,867

Ileje	2,010	1,918	1,857
Kyela	2,012	1,921	1,860
Mbarali (Rujewa)	1,981	1,889	1,828
Mbozi (Vwawa)	2,006	1,914	1,853
Momba (Chitete)	2,015	1,923	1,862
Rungwe (Tukuyu)	2,006	1,914	1,853
Morogoro	1,915	1,823	1,762
Mikumi	1,930	1,839	1,777
Kilombero (Ifakara)	1,952	1,861	1,800
Kilombero (Mlimba)	1,975	1,883	1,822
Kilombero (Mngeta)	1,964	1,872	1,811
Ulanga (Mahenge)	1,963	1,872	1,810
Malinyi	1,973	1,882	1,820
Kilosa	1,933	1,842	1,780
Gairo	1,933	1,842	1,780
Mvomero (Wami Sokoine)	1,925	1,834	1,772
Turian	1,940	1,848	1,787
Mtwara	1,962	1,870	1,809
Nanyumbu (Mangaka)	2,011	1,919	1,858
Masasi	1,988	1,896	1,835
Newala	1,994	1,902	1,841
Tandahimba	1,987	1,896	1,834
Mwanza	2,040	1,948	1,887
Kwimba	2,076	1,984	1,923
Magu	2,048	1,956	1,895
Misungwi	2,045	1,954	1,892
Sengerema	2,072	1,980	1,919
Ukerewe	2,099	2,007	1,946
Sumbawanga	2,062	1,971	1,909
Kalambo (Matai)	2,055	1,963	1,902
Nkasi (Namanye)	2,076	1,984	1,923
Katavi (Mpanda)	2,097	2,006	1,944
Mlele (Inyonga)	2,076	1,984	1,923
Songea	2,013	1,921	1,860
Mbinga	2,046	1,955	1,894
Namtumbo	2,042	1,951	1,889
Nyasa (Mbamba Bay)	2,049	1,957	1,896
Tunduru	2,072	1,980	1,919
Shinyanga	2,018	1,927	1,865
Kahama	2,032	1,940	1,879
Kishapu	2,047	1,955	1,894
Simiyu (Bariadi)	2,060	1,968	1,907
Busega (Nyashimo)	2,053	1,961	1,900
Itilima (Lagangabilili)	2,063	1,971	1,910
Maswa	2,051	1,960	1,898

Meatu (Mwanhuzi)	2,058	1,967	1,905
Singida	1,980	1,889	1,827
Iramba	1,992	1,901	1,839
Manyoni	1,965	1,873	1,812
Ikungi	1,976	1,884	1,823
Mkalama (Nduguti)	2,005	1,913	1,852
Tabora	2,044	1,952	1,891
Igunga	1,998	1,906	1,845
Kaliua	2,062	1,970	1,909
Ulyankulu	2,056	1,964	1,903
Nzega	2,008	1,917	1,855
Sikonge	2,055	1,964	1,903
Urambo	2,057	1,965	1,904
Tanga	1,854	1,705	1,656
Handeni	1,875	1,725	1,677
Kilindi	1,890	1,740	1,692
Korogwe	1,866	1,717	1,669
Lushoto	1,876	1,726	1,678
Mkinga (Maramba)	1,861	1,712	1,663
Muheza	1,859	1,709	1,661
Pangani	1,861	1,711	1,663

B: BEI ZA JUMLA

Bei za Jumla - DSM	Petroli (Sh/L)	Dizeli (Sh/L)	Mafuta ya Taa (Sh/L)
Bei Kikomo	1,781.75	1,690.16	1,628.93

Bei za Jumla-TANGA	Petroli (Sh/L)	Dizeli (Sh/L)	Mafuta ya Taa (Sh/L)
Bei Kikomo	1,746.22	1,596.65	1,548.48

Felix Ngamlagosi

MKURUGENZI MKUU
EWURA